

Swahili transcript:

Nitazungumza kuhusu historia ya maisha yangu. Mimi nilizaliwa katika jiji la Dar es salaam, na wakati bado nipo mtoto mdogo, mama yangu mkubwa ambaye anaishi mkoa wa Ruvuma, mkoa wa Ruvuma uko kusini mwa nchi ya Tanzania, alinichukua ili kunilea, kwa hiyo nilianza kuishi na mama yangu huyu mkubwa nikiwa bado mtoto mdogo, kwa hiyo nilipofikia umri wa kwenda chekechea, nikaanza chekechea nikasoma kwa miaka mitatu. Na nilipokuwa na umri wa miaka sita walinipeleka shule ya msingi, kwa hiyo nilianza darasa la kwanza. Nakumbuka wakati tunaanza darasa la kwanza kipindi kile ni kwamba tulikuwa tunaandika kwanza chini kwenye vumbi, unaandika, mwalimu anakuja anaangalia kama umeandika vizuri, unapewa ubao, unapewa ubao pamoja na chaki, unaandika pale. Ukiweza kuandika vizuri katika ule ubao, ndipo unapewa daftari pamoja na kalamu. Ukiweza kuandika vizuri katika daftari kwa kutumia kalamu, ndipo ambapo unaruhusiwa sasa kutumia kalamu ya wino, hiyo ya kwanza ilikuwa ni penseli, lakini unapofikia umefanya vizuri katika kuandika kwa penseli, unapewa sasa kalamu ya wino. Kwa hiyo nikikumbuka maisha haya ninapata changamoto kubwa sana hasa katika maisha ya sasa ambapo wanafunzi wanakwenda shule darasa la kwanza tayari anajua kutumia kompyuta kwa mfano ambao wana uwezo ambao wanawapeleka watoto wao katika shule za watu binfsi ambazo lugha ya kufundishia ni lugha ya kiingereza, kwa hiyo utakuta wanajifunza kompyuta wakiwa bado watoto wadogo. Hiyo ilinipa changamoto sana ya kuweza kusoma na kuweza kufanya vizuri katika mitihani yangu. Kwa hiyo nilijitahidi na nilipofika darasa la saba nikachaguliwa kwenda shule ya sekondari. Nilikwenda nilisoma shule inaitwa shule ya sekondari ya wasichana Songea. Kufika kule mwalimu wetu wa kiingereza alikuwa anatusisitiza sana tujifunze lugha ya kiingereza, lakini kutokana na msingi ule ambao tulikuwa nao wa kutumia lugha ya kiswahili toka tulipokuwa chekechea, kidogo ilikuwa ngumu kuweza kumudu masomo ya sekondari lakini tulikuwa tunajitahidi, na nilipomaliza form four, aah! darasa la kumi na mbili nikafaulu vizuri na nikachaguliwa kwenda high school, na nilisoma Zanaki, ambayo ipo Dar es salaam, na nilipofika Zanaki, niliweka malengo kwamba ninataka nifike mpaka chuo kikuu, sababu kaka yangu mkubwa alikuwa anasoma wakati huo katika chuo kikuu cha Dar es salaam na alipokuwa anakuja likizo, alikuwa anatupa habari nyingi sana za chuo kikuu, kwa hiyo nilihamasika sana kuwa siku moja na mimi niweze kufika chuo kikuu. Kwa hiyo nikajitahidi sana katika masomo yangu nikiwa Zanaki na kwa bahati nzuri nilipomaliza kidato cha sita, nilipata daraja la kwanza na nilifurahi sana. Nika-apply chuo kikuu, niliandika maombi kwa ajili ya kujiunga na chuo kikuu cha Dar es salaam na kwa bahati nzuri nikachaguliwa na nilisoma katika chuo

kikuu cha Dar es salaam toka ule mwaka wa elfu moja mia tisa tisini na saba na nilipata shahada ya ualimu mwaka elfu mbili na moja, ndipo ambapo nilimaliza elimu yangu ya chuo kikuu, chuo kikuu cha Dar es salaam. Kwa hiyo ninafurahi sana kwa sasa mimi ni mwalimu na nina watoto wawili, nimeolewa, mume wangu anaitwa Sixfrid, tulikutana na Sixfrid nikiwa nasoma chuo kikuu cha Dar es salaam, yeye alikuwa anasomea uhandisi na mimi nilikuwa nasomea ualimu. Kwa hiyo tukawa marafiki na akanichumbia na baadae alinioa mwaka ule wa elfu mbili wakati namaliza elimu yangu ya chuo kikuu. Kwa hiyo nimefurahi sana kwa vile nilifanya vizuri na nikaweza kuchaguliwa kwenda kufundisha shule ya sekondari Dar es salaam, shule inaitwa Benjamin Wiliam Mkapu, na baadae nikahamishiwa shule ya sekondari Dodoma, ambayo iko mkoa wa Dodoma. Tulihamia Dodoma kwa vile mume wangu alihamishiwa kikazi mkoa wa Dodoma, tulikuwa tunaishi jiji la Dar es salaam, na baadae akahamishiwa mkoa wa Dodoma, kwa hiyo wote sasa tukahamia mkoa wa Dodoma, kwa hiyo tunaishi kule, familia yangu iko mahali pale.

English translation:

I would like to talk about my life story. I was born in Dar es Salaam city and was raised by my aunt who lives in Ruvuma region. Ruvuma region is located at the southern part of Tanzania. When I reached the age of going to nursery school, I was sent to school. I started nursery school and went for three years. When I was six, I started primary school (elementary school). At that time, when students start standard one, they first write in the dust. Then the teacher comes to see your handwriting. If she/he is satisfied with your handwriting, they offer you a small blackboard and a chalk and you write on it. If your handwriting is good, they offer you an exercise book with a pencil. Finally, if your handwriting is better, they allow you to use an exercise book with a pen. When I remember these things, I am a little envious when I see students going to standard one who already know how to use a computer. This is especially true for those whose parents are rich and can afford to send their children to private schools where the medium of instruction from kindergarten on up is in English. They learn how to use computers when they are still young. That inspired me a lot to study hard and finally I performed well in my exams and was selected to join secondary school/middle school. I went to Songea Girls secondary school. While at Songea Girls, our English teacher encouraged us to study hard and use the English language. However, because of my poor background in using the Swahili language since nursery school, that was a big challenge for my studies. The medium of instruction in secondary education was English. With a lot of effort, I performed well and was selected to attend high school. I

went to Zanaki high school in Dar es Salaam. When I was at Zanaki, I decided to study hard so that I could go to the university after high school. At that time, my brother was studying at the University of Dar es Salaam. During vacation, he used to tell us many stories about university studies, so that encouraged me a lot to study hard. At Zanaki, I studied very hard and after my final exams, I got the first grade, and I was very happy. So I applied to the University of Dar es Salaam, and I was selected to enter there. I began my studies at the university in 1997, and I received Bachelor of Arts with Education in the year 2001. Now I am happy because I am a teacher. I am married and I have two children. My husband is called Sixfrid Jacob. I met him when he was doing his Bachelor of Science in electrical engineering. He proposed and I accepted, and we got married two year later when I was finishing my studies at the university in 2000. After my graduation, I was selected to teach at Benjamin William Mkapa high school in Dar es Salaam. In January, 2006, we got a transfer to Dodoma region, and I now teach at Dodoma high school. For now, my family lives there.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated